# MAELEZO KWA JAMII KUHUSU KUONGEZA THAMANI YA MISITU YA VIJIJI KUPITIA UTHIBITISHAJI WA MAZAO YA MISITU

## Dhana ya uthibitishaji ni nini?

Ni mchakato unaotoa uhakika kwamba alama na vielelezo vinatolewa kuonyesha kuwa bidhaa ya misitu imetoka kwenye msitu uliotunzwa vizuri/endelevu.

- Ni uthibitisho kwamba kuna uhifadhi mzuri na matumizi mazuri yanayozingatia na kufuata misingi endelevu.
- Uthibitishaji unazingatia Sera nzuri inayoongoza uzalishaji.
- Inathibitisha kuwa wadau wanatunza vizuri msitu na mwenye kiwanda anachakata vizuri mazao ya misitu kwa kufuata taratibu na sheria zilizopo.
- Uthibitishaji unatoa uhakika kwa wateja kuwa mazao wanayonunua yataendelea kuwepo.

## Kwa nini uthibitishaji wa mazao ya misitu?

- Uthibitishaji unavutia na kufungua mianya mipya ya masoko ya uhakika ya ndani na nje.
- Uthibitishaji unahamasisha utunzaji na uhifadhi wa misitu kwa ubora zaidi.
- Ni dhana ya kufanikisha maendeleo endelevu kwa jamii na kwa taifa .
- Chombo cha utekelezaji wa sera zetu hasa ile ya uendelezaji wa misitu.
- Dhana ya kuvutia ushirikishwaji wa jamii katika utunzaji na uendelezaji wa misitu kupitia usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii UMJ (Usimamizi wa Misitu ya Jamii) na Usimamizi wa pamoja wa misitu (JFM).
- Chombo cha mawasiliano – kati ya wanunuzi, jamii, na asasi mbalimbali.
- Ni dhana ya kupunguza umaskini – kupitia MKUKUTA na MKURABITA.
- Uthibitishaji una mlengo wa kiuchumi zaidi katika, shughuli zote za utunzaji na uendelezaji misitu umeelekezwa zaidi katika biashara na kupata faida.
- Uthibitishaji una unganisha dhana ya uhifadhi inavyowiana na maendeleo ya jamii husika.

## Uthibitishaji una malengo makuu mawili:-

- Kichocheo cha masoko na kuboresha uhifadhi wa misitu.
- Kuboresha masoko na kuongeza mrahaba.

Uthibitishaji ni chombo cha kiuchumi na unaorahisisha uhifadhi wa misitu kulingana na viwango vilivyowekwa na kukubalika.

## Faida za uthibitishaji wa mazao ya misitu:-

### Kimazingira

- Uboreshaji wa uhifadhi kwa kutoa faida kwa watunzaji wa msitu.
- Kuwepo na uwazi na kudhibiti kwa rasilimali ya maliasili.

### Kijamii

- Unapunguza mgogoro kwani kunakuwa na makubaliano ya misingi ya kuhifadhi.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

WITO KWA WANAMITANDAO NA JAMII ZOTE:
Ifahamike kwamba vijiji, jamii na mitandao yote nchini Tanzania ambayo inatekeleza mpango wa utunzaji na uhifadhi wa Misitu kwa njia ya ushirikishwaji katika Misitu ya hifadhi wanaweza kujiunga katika cheti cha kikundi cha uthibitishaji ili mradi tu watapitia mchakato unaotakiwa na FSC na kuweza kufikia viwango vinavyotakiwa.

© WWF ®

- Uthibitishaji unaheshimu mambo ya kijamii.

**Kiuchumi**

- Ugawanyaji ulio wazi wa mapato, hakuna kupunja wala kupunjwa.
- Masoko ya uhakika kwa wateja ambao wanataka kuingiza au kununua bidhaa zilizothibitishwa tu.
- Wateja wa sasa wanataka bidhaa zilizotoka kwenye msitu inayosimamiwa kwa njia endelevu.

## Hatua za kufanya ili bidhaa za misitu yenu ziweze kudhibitishwa:-

- Uamuzi wa nini kithibitishwe kama vile miti, mazao yasiyo timbao (asali, uyoga, mkaa), utalii, n.k
- Kuchagua mthibitishaji ambaye hana maslahi kwa namna yoyote kwa mthibitishwaji.
- Utambuzi wa wadau wanaokufahamu.
- Vikundi vya kiraia.
- Tathimini shirikishi ya rasilimali inayothibitishwa.
- Mafunzo kwa jamii juu ya utunzaji wa misitu na uthibishaji, masharti yake.
- Uwekaji wa kumbukumbu.

## Aina za Uthibitishaji wa msitu na mazao yake:

1. Upande wa utunzaji na uhifadhi wa msitu (Meneja wa msitu)

- Huangalia shughuli endelevu za utunzaji na uhifadhi kwenye msitu husika.

2. Upande wa mazao ya msitu (Kiwanda cha kuchakata mazao ya misitu)

- Unahusisha ufuatiliaji wa namna taratibu endelevu zinavyofuatwa katika kuchakata mazao ya msitu (chain of custody) kutoka msituni kupitia kiwandani hadi kwa mteja.

## Tunajifunza nini kuhusu hii dhana nzima ya uthibitishaji wa mazao ya misitu ya jamii?

- Uthibitishaji ni chombo kizuri cha kuhamasisha utunzaji wa misitu.
- Uthibitishaji unatoa mahitaji ya jamii zaidi ya kuwa na misitu ya ikolojia pekee.
- Maswala ya kiuchumi na kijamii yana tambulika katika mpango wa uthibitshaji.
- Ushirikiano wa wadau ni mzuri katika mpango wa uthibitshaji.

Mifano ya miradi ya uthibitishaji inayoendelea na aina ya vyeti, Tanzania

- Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo (MCDI) – Cheti cha FSC: Vijiji 6 vyenye misitu ya hifadhi ya vijiji vimepata cheti cha kikundi cha jamii kuhusu utunzanji na uhifadhi bora wa misitu. Vijiji hivyo ni Nainokwe, Kikole, Liwiti na Kisangi toka wilaya ya Lindi na Tawi na Nyamwage kutoka wilaya ya Rufiji.
- Kampuni ya TANWAT – Cheti cha mashamba ya miti – FSC.
- Kampuni ya Mitiki: KVTC – SA bureau of Standards & ISO.
- Kampuni ya Green Resources Limited – FSC & ISO.
- Kampuni ya Kiwanda cha mbao ya Sandali Wood iliyoko Tanga ina cheti cha FSC cha uchakataji mazao ya misitu.
  Mwakilishi wa FSC nchini Tanzania Ndg Severine Kalonga ameshateuliwa na ameshaanza kazi ya ushauri kuhusu uthibitishaji wa mazao ya misitu nchini.

## Gharama za kuingia kwenye mchakato huu zipoje?

Katika hatua za awali mchakato huu huwa na gharama kubwa. Hata hivyo, wakala wa Misitu Tanzania kwa kushirkiana na shirika la WWF na wadau wengine wanashughulikia kupata kanuni zetu za taifa za FSC za uthibitishaji wa mazao ya misitu. Uwepo wa kanuni hizi utapunguza gharama kwa kiasi kikubwa. Kanuni zipo katika hatua za mwisho.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
WWF Tanzania, S.L.P 63117, Dar es Salaam
Simu: 022 2700077, Baruapepe: psumbi@wwftz.org

SNAL